African Population and Health Research Center
Transforming lives in Africa through research.

hakielimu

Muhtasari wa Utafiti

Upatikanaji wa Elimu Bora kwa Watoto Wanaoishi Katika Makazi Duni Mijini nchini Tanzania

Nyambura Thiong'o, Francis Kiroro, Moses Ngware, Wilberforce Meena, Rose Kalage na John Kalage

Utangulizi

Elimu kwa watoto wa mijini inaibuka kuwa mada muhimu ya mjadala nchini Tanzania na nchi nyingine za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara 'SSA', hasa kutokana na changamoto zinazowakabili watu wanaoishi kwenye makazi duni katika maeneo ya mijini. Wanafunzi kutoka kaya za kipato cha chini wanaoishi mazingira duni ya mijini hukumbana na matatizo mengi kwenye safari yao ya kupata elimu ikilinganishwa na wenzao waliotoka familia za kipato cha kati na kipato cha juu. Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, inakabiliwa na ukuaji mkubwa wa miji, unaoashiria ongezeko kubwa la uhamiaji kutoka vijijini kwenda mijini. Kidunia, Tanzania ni nchi ya sita yenye kiwango cha juu zaidi cha ongezeko la watu mijini (Worrall et al., 2017). Hali hii inatarajiwa kuendelea, na inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2050, asilimia 55 ya watu wa Tanzania watakuwa mijini (Benki ya Dunia, 2016), huku Dar es Salaam ikiongoza kwa ongezeko la watu mijini barani Afrika (Kielelezo 1).



Kielelezo cha 1: Ukuaji wa Majiji nchi za Afrika. Chanzo:"Africa Progress Group"

Kuelewa hali ya sasa ya elimu ya watoto waishio mijini ni muhimu ili kuandaa mipango ya kushughulikia mahitaji yanayoongezeka ya elimu mijini kwa siku zijazo. Muhtasari huu unawasilisha matokeo muhimu ya utafiti wa elimu ya watoto kutoka familia maskini waishio mijini. Utafiti uliangalia mwelekeo wa utoaji elimu kwa watoto wanaoishi maeneo ya mijini kutoka familia maskini na kuongeza ukuaji wa miji ya Tanzania.

Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

1. Je, kuna mwelekeo upi wa elimu kwa watoto wanaoishi mjini wanaotoka kaya maskini nchini Tanzania - ikiwa ni pamoja na wale wenye mahitaji maalum?

2. Je, jamii maskini za mijini zinafahamu nini kuhusu elimu kama haki katika muktadha wa ukuaji wa miji nchini Tanzania?

3. Je, kuna fursa gani za elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum na wanaoishi kaya maskini maeneo ya mijini?

Mbinu ya Utafiti na Maeneo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusanya data kutoka vyanzo na sehemu mbalimbali kwa kutumia mbinu mchanganyiko (mbinu za kitaamuli na kitakwimu). Utafiti huu ulilenga kaya zenye watoto wanaosoma shule, wenye umri kati ya miaka 3 hadi 19 wanaoishi makazi yasiyo rasmi mijini mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma. Maeneo hayo yalichaguliwa kwa kuzingatia vigezo viwili vikuu. Kwanza, idadi kubwa ya wakazi wa kipato cha chini wa mijini na pili eneo liwe linatambulika kama eneo la wakazi wenye kipato cha chini. Takwimu zilikusanywa kutoka kaya 1,200 za wananchi wenye kipato cha chini zilizochaguliwa kinasibu. Pia walihojiwa wakuu wa shule 98 ambako wanasoma watoto kutoka kaya zenye kipato cha chini zilizochaguliwa.

Takwimu za kiasi zilipatikana kupitia majadiliano ya vikundi mjadala na walezi/wazazi. Pia mahojiano ya kina na mahojiano na watoa taarifa muhimu yalifanyika kwa kuwahusisha viongozi na watunga sera. Uchambuzi wa data ulifanywa kwa idadi ya watoto 2,150 wenye umri wa miaka 5-17, ambao ni umri elekezi kwa elimu ya lazima nchini Tanzania. Alama za hali ya kipato, zilichukuliwa kwa kuangalia mali inazomiliki kaya, ziliainishwa kwenye makundi matatu sawa kwa madhumuni ya kurahisisha uchanganuzi. Jedwali 1 linaonesha mtawanyiko wa kaya ndani ya maeneo ya utafiti na sifa za kaya- Jedwali la 2.

Jedwali la 1: Mtawanyiko wa Kaya kwenye Maeneo ya Utafiti

Ngazi	Eneo la Utafiti	Idadi ya Kaya	Asilimia
Mkoa	Dar es Salaam	814	67.8
	Dodoma	386	32.2
Wilaya	Dodoma Municipal	386	32.2
	Illala	236	19.7
	Kinondoni	266	22.2
	Temeke	312	26.0
Kata	Chang'ombe	386	32.2
	Hananasifu	266	22.2
	Kiburugwa	312	26.0
	Kipawa	236	19.7
Mtaa/Kijiji	Hamvu	149	12.4
	Hananasifu	140	11.7
	Juhudi	107	8.9
	Karakata	95	7.9
	Kawawa	126	10.5
	Kiburugwa kwa Nyoka	123	10.3
	Kiburugwa namba tatu	82	6.8
	Kishoka	105	8.8
	Mazengo	132	11.0
	Mji Mpya	141	11.8
Jumla		**1200**	**100.0**

Jedwali la 2: Sifa za Kaya

	Jumla (% ya kaya 1,200)	**Kipato cha Chini** (% ya kaya 396)	**Kipato cha Kati** (% ya kaya 398)	**Kipato cha Juu** (% ya kaya 406)
Ukubwa wa Kaya				
Wanafamilia 2-3	20.6%	22.8%	20.6%	18.4%
Wanafamilia 4-5	44.8%	45.5%	44.9%	44.1%
Wanafamilia 6-7	21.8%	19.7%	21.8%	24.0%
Wanafamilia 8-21	12.7%	12.0%	12.6%	13.5%
Elimu ya Mkuu wa Kaya				
Hakusoma/nyingine	5.9%	10.3%	6.0%	1.4%
Msingi	69.8%	73.6%	76.1%	59.7%
Sekondari	20.2%	14.2%	16.9%	29.5%
Kati/Juu	4.1%	1.9%	1.0%	9.5%
Jinsi ya Mkuu wa Kaya				
Mwanamke	35.9%	49.8%	34.8%	23.3%
Mwanaume	64.1%	50.2%	65.2%	76.7%
Umri wa Mkuu wa Kaya(miaka)				
Chini ya 40	40.8%	43.0%	42.2%	37.3%
Miaka 40-49	29.6%	28.6%	30.0%	30.3%
Miaka 50-59	14.0%	11.8%	14.0%	16.2%
Miaka 60 na zaidi	15.6%	16.6%	13.8%	16.2%
Hali ya ndoa ya mkuu wa kaya				
Ameoa/kaolewa, wake wengi, mke mmoja	71.2%	59.2%	73.8%	80.6%
Mjane	13.3%	18.5%	12.4%	8.9%
Walitengana/mtalaka	8.5%	12.1%	9.3%	4.1%
Hakuwahi kuolewa	7.0%	10.2%	4.5%	6.3%

Maelezo: * Mwenye umri mdogo zaidi alikuwa na miaka 22.

Takriban wakuu wa kaya 7 kati ya 10 (70%) wamekomea elimu ya msingi. Kwa ujumla, kaya nyingi zinaongozwa na wanaume kama wakuu wa kaya (64%). Zaidi ya theluthi mbili ya kaya (70.4%) zinaongozwa na wakuu wa kaya wenye umri chini ya miaka 50. Wengi wao (58%) walikuwa na umri chini ya miaka 40.

Kutokana na Jedwali namba 3, watoto wengi (50%) wenye umri wa kati ya miaka 5-17 kwenye maeneo ya utafiti walikuwa na umri wa kwenda shule ya msingi miaka 7-13, wakifuatiwa na wenye miaka 14-17 (25%) na miaka 5-6. (14.6%). Kwa ujumla, kulikuwa na wasichana wengi zaidi kuliko wavulana.

Jedwali la 3: Sifa za Watoto wenye Umri miaka 5 - 17

	Jumla (2,150)	**Asilimia ya alama ya hali ya kipato cha kaya ya mtoto**		
		Kipato cha Chini (% ya 723)	Kipato cha Kati (% ya 730)	Kipato cha Juu (% ya 697)
Umri wa mtoto kwa miaka				
Miaka 5-6	14.6%	13.6%	15.8%	14.4%
Miaka 7-13	60.4%	62.3%	58.0%	61.1%
Miaka 14-17	25.0%	24.2%	26.3%	24.4%
Wastani wa umri (inaendelea)	10.5	10.6	10.5	10.5
Jinsi ya Mtoto				
Wa kike	50.5%	50.7%	49.8%	50.8%
Wa Kiume	49.5%	49.3%	50.2%	49.2%
Hali ya uyatima wa mtoto				
Wazazi wote wako hai	86.3%	85.8%	85.1%	88.2%
Wazazi wote wamefariki	1.9%	1.6%	2.1%	2.0%
Mzazi mmoja yuko hai	11.7%	12.6%	12.8%	9.7%
Mtoto ana ulemavu/mahitaji maalum	2.5%	2.0%	3.0%	2.5%

Jumla ya sampuli za shule zilizofikiwa na utafiti huo zilikuwa ni 98; shule 79 za mkoa wa Dar es Salaam na Shule 19 za Dodoma. Kati ya shule hizo zilizofikiwa, 68% zilikuwa za umma, na 32% shule binafsi Kati ya 32% ya shule za binafsi, 81% ni shule za awali.

Matokeo ya Utafiti

Watoto kwenda shuleni

Matokeo yanaonesha kuwa kwa ujumla, 98.1% ya watoto wamewahi kwenda shule. Kijinsia, wasichana wengi zaidi wanakwenda shule ikilinganishwa na wavulana – faharasa ya usawa wa jinsia ilikuwa 1.02. Vile vile, matokeo yanaonesha kuwa wasichana wote (100%) wamesoma shule za awali tofauti na wavulana ambao ni 95.5% tu. Mwenendo huo uko shule za msingi na sekondari ambapo wasichana huhudhuria zaidi masomo shuleni. Hata hivyo, ni vyema kutambua kuwa kiwango cha watoto kwenda shule kilikuwa kikipungua (kwa wavulana na wasichana) kadri miaka ilivyokuwa inongezeka, na kupungua zaidi kulionekana kwa wanafunzi wa sekondari. Pia utafiti uliangalia watoto wenye ulemavu. Utafiti ulibaini kuwa kati ya watoto 2,150, watoto 56 (2.3%) walikuwa wanafunzi wenye ulemavu. Kati ya watoto 56 waliokuwa na ulemavu (19.3%) walikuwa na ulemavu wa viungo, 17.2% walikuwa viziwi, 13% walikuwa na uoni hafifu, wakati 8.4% walikuwa na ulemavu wa akili. Miongoni mwa watoto hao wenye ulemavu, wavulana wengi zaidi (10.2%) waliandikishwa shuleni, kuliko wasichana (9.2%).



Kielelezo 2: Aina ya mahitaji maalumu/ulemavu miongoni mwa watoto wenye umri miaka 5-17 (N=57)

Mchangamano au ujumuishi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum/ulemavu

Utafiti ulibaini kuwa shule 6 kati ya 10 zilikuwa zimeweka mazingira rafiki na huduma kwa wanafunzi wenye ulemavu. Shule ambazo ziliripoti kuwa hazina huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum zilikuwa na vifaa duni vya kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum. Aidha, utafiti ulitaka kuelewa zaidi jinsi shule zenye huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum zilivyokuwa zikiwahudumia watoto wenye ulemavu. Karibu shule zote za kawaida (94.7%) zilikuwa na madarasa mchanganyiko kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Uandikishaji kwa aina ya Shule na ngazi ya elimu

Kwa ujumla, watoto wengi 87% wameandikishwa shule za umma. Pia ni muhimu kufahamu kuwa watoto walioandikishwa kwenye shule za binafsi wengi wao ni ngazi ya awali (20%) ikilinganishwa na shule za msingi (13%) na sekondari (9.4%). Sababu kubwa zilizowafanya wazazi wachague shule fulani ni unafuu wa gharama (wanapendelea zile za bei nafuu), ukaribu wa kufikika, na ufaulu bora wa shule.



Kielelezo 3: Sababu zinazowafanya wazazi wachague kuandikisha watoto shule binafsi au shule za umma.

Uandikishaji wa jumla na uandikishaji halisi

Uandikishaji Halisi shule za msingi 'NER' ulikuwa 83.7%, hii inaonesha kuwa 16.3% ya watoto wenye umri wa kwenda shule ya msingi kutoka kaya zilizoshiriki hawakuwa shuleni. Kwa shule za Sekondari, Undikishaji wa Jumla 'GER' na Undikishaji Halisi 'NER' ulikuwa chini ya 100%, kwa 89.8% na 71.6%, mtawalia. Hii ina maana kuwa kuna wanafunzi wengi wanakatisha masomo wakiwa shule za msingi na sekondari maeneo ya mijini katika kaya za watu maskini nchini Tanzania.

Faharasa ya usawa wa kijinsia 'GPI'

Kwa ujumla, utafiti ulibaini kuwa kulikuwa na usawa wa kijinsia kwa wasichana na wavulana shule ya msingi (1.00) katika maeneo yaliyofikiwa. Hata hivyo, kulikuwa na tofauti katika ngazi ya sekondari wasichana walikuwa wengi zaidi (1.06). Mwenendo huu unakubaliana na ripoti ya UNESCO (2021) inayosema kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa ya Faharasa ya Usawa wa Jinsia kwenye uandikishaji wa jumla shule za sekondari, kutoka 0.96 mwaka 2014 hadi 1.10 mwaka 2020.

Wanafunzi kurudia darasa

Wahojiwa walisema sababu kuu za wanafunzi wa umri kati ya miaka 5-13 kurudia darasa ni pamoja na: wanafunzi kushindwa kufikia wastani wa ufaulu uliopangwa ili kuvuka darasa (54.8%), wazazi kuhamia maeneo mengine (9.9%), na watoto kuhamishiwa shule nyingine (4.8%); kwa wale wenye umri wa miaka 14-17 sababu zilikuwa: kutofikia wastani wa ufaulu uliopangwa (85.8%), umri mdogo sana kuhamia darasa la juu (9.5%) na kuhamishiwa shule nyingine (4.8%). Matokeo ya viwango vya ufaulu yanaonesha kuwa kwa wastani, wavulana wengi zaidi walirudia darasa kuliko wasichana. Viwango vya wanafunzi kuvuka ngazi moja ya darasa kuhamia ngazi ya juu vilikuwa zaidi ya 98% ikimaanisha kuwa kiwango cha wanafunzi kuacha shule ni kidogo sana miongoni mwa wanafunzi wanaotoka familia duni maeneo ya mijini.

Sifa za Walimu

Kwa ngazi ya shule za msingi, walimu wengi wa kike walikuwa na elimu ya ualimu ngazi ya cheti (57.8%) wakati wenzao wanaume chini ya nusu pia walikuwa na cheti cha ualimu (36.5%). Kwa sifa ya Stashahada, wanaume wengi zaidi (24.6%) kuliko wanawake (18.3%) walikuwa na sifa hii. Kwa shule za sekondari, walimu wengi walikuwa na elimu ya ualimu ngazi ya shahada, na walimu wanawake ni wengi zaidi wenye shahada (71.5%) ikilinganishwa na walimu wa kiume (65.6%). Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo ya Elimu Maalum kwa ngazi za shule za msingi na sekondari ilikuwa ndogo sana, ni chini ya 1% kwa ngazi zote. Ingawa ni jambo la kupongezwa kwamba walimu wengi, wa jinsia zote, wana sifa za kutosha za kitaaluma, utafiti unaonesha bado juhudi kubwa zinahitajika kupata walimu wenye sifa kwa ajili ya elimu maalum.

Uwiano wa Kitabu cha Kiada kwa Mwanafunzi

Kwa ujumla utafiti ulionesha ikama iko juu zaidi kuliko inavyopaswa kuwa kwa ngazi zote, kuanzia shule ya awali hadi sekondari. Ikama ni kubwa zaidi shule za msingi (takriban wanafunzi 53 kwa kila mwalimu). Hii inapunguza ufanisi na kuathiri ubora wa elimu. Pia huongeza mzigo kwa walimu hasa wakati wa kusahisha kazi za wanafunzi na mitihani yao.

Jedwali la 4: Uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi kwa ngazi ya shule

Ngazi ya shule	Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi	Idadi ya shule
Awali	43.2	14
Msingi	52.6	32
Sekondari	47.6	34

Wastani wa ukubwa wa darasa

Utafiti huu ulibaini kuwa ukubwa wa madarasa unatofautiana kulingana na ngazi ya darasa. Madarasa ya watoto wadogo (Chini ya miaka 1-2 na 3-4) ni madogo (yana wastani wa watoto 5-21 kwa kila darasa), lakini darasa la awali ngazi ya juu, madarasa yake ni makubwa zaidi hadi watoto (67). Ukubwa wa madarasa uliendelea kuongezeka zaidi kwa madarasa ya msingi. Mathalani, darasa la kwanza (136), darasa la pili (watoto wengi zaidi hadi 144) na darasa la tatu (134). Lakini, jambo la kuvutia ni kwamba ukubwa wa madarasa ulianza kupungua tena kuanzia darasa la nne (119) na hali ya kushuka iliendelea hadi darasa la Saba (104). Kwenye shule za sekondari, ukubwa wa madarasa ulikuwa juu sana kwa kidato cha kwanza (111) na cha pili (103), lakini ukubwa wa madarasa ulipungua sana kwa kidato cha tatu (76) na kidato cha nne (78).

Uwiano wa Kitabu kwa Mwanafunzi

Utafiti ulilenga kuchunguza masomo matatu makuu: Kiingereza, Kiswahili na Hisabati ambayo ni msingi wa kukuza umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Utafiti uligundua kuna uwiano mkubwa wa vitabu vya wanafunzi kwa ujumla katika shule za msingi na sekondari. Kwa mfano, uwiano wa vitabu vya kiada kwa wanafunzi ni takriban 30:1 kwa somo la Hisabati darasa la tatu. Uwiano mdogo japo haujafikia uwiano unaotakiwa ulionekana kwa darasa la nne na la sita ambao ni karibu 7:1 na 6:1 mtawalia. Darasa la Saba lilikuwa na uwiano mdogo kabisa wa vitabu vya kiada kwa wanafunzi takriban 2:1 kwa masomo yote matatu.

Wazazi/walezi kuwasaidia watoto kazi za masomo nyumbani na masuala ya shuleni

Wanafunzi wa madarasa ya chini (elimu ya awali) walipata msaada mkubwa zaidi toka kwa wazazi/walezi kukamilisha kazi zao za masomo, lakini wenzao wa sekondari walipata msaada mdogo sana. Wazazi wengi pia hawakuweza kushiriki kwenye shughuli nyingine za shule kama vile kukutana na walimu ili kujadili maendeleo ya watoto wao shuleni. Kwa upande mwingine, baadhi ya wazazi walieleza kutoridhishwa kwao na baadhi ya tabia za walimu zinazoathiri ubora wa ujifunzaji kama vile kutilia mkazo twisheni za nje ya masomo.

Upatikanaji wa Maji safi, usafi wa mazingira na kulinda afya

Utafiti uligundua kuwa karibu 20% ya shule hazina vifaa vya kunawia mikono vinavyofanyakazi. Pia, kati ya shule hizo 67, asilimia 65.7 (shule 44) zilikuwa na vyoo vya kuvuta maji na 98.5% ya vyoo hivyo viko ndani ya eneo la shule. Aidha, 98.5% (shule 66) shule ziliripoti kuwa vyoo hivi pia vilikuwa vimetenganishwa, kama inavyotarajiwa, kwa ajili ya wavulana na wasichana. Shule nyingi zilikuwa na vyoo kwa ajili ya walimu na wafanyakazi (97%), shule wachache sana (3%) ziliripoti kuwa vyoo vyao vinatumiwa na wote -walimu na wanafunzi. Kuhusu uwiano wa Choo kwa Mwanafunzi, utafiti uligundua uko 50:1. Kuhusu uwepo wa vyoo maalum kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, ni shule chache tu 26.9% (shule 18) ndizo ziliripoti kuwa zina vyoo maalum, rafiki na vinavyotumika kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Utawala, Menejimenti na Uthibiti wa Ubora

Shule nyingi ziliripoti zimewahi kutembelewa na Wathibiti ubora wa shule mara moja tu kwa mwaka (44.8%) au mara mbili kwa mwaka (29.9%). Takriban 14.9% ya shule, ziliripoti kuwa hazijawahi

kutembelewa na Wathibiti ubora wa shule. Matokeo haya yanaashiria kuwa bado kuna haja ya serikali kuhakikisha wathibiti ubora wa shule na maafisa Afya wanafika shuleni mara kwa mara ili kuhakiki ubora na kulinda viwango vinavyotarajiwa kwenye ujifunzaji, usalama na afya.

Maoni ya Wadau kuhusu dhamira ya Serikali Kuhakikisha Haki ya Elimu

Serikali ya Tanzania imejitahidi sana kuhakikisha wananchi wote wanapata elimu. Hii inaungwa mkono na mada ndogo tatu zilizoibuka wakati wa majadiliano sera na mikakati, utekelezaji wa sheria, na mpango wa lishe shuleni.

Sera na Mikakati ya Kusaidia Utekelezaji Haki ya Elimu: Wadau hao walitaja sera ya elimu bila ada kwa elimu ya msingi na sekondari kama mfano wa juhudi za Serikali za kuhakikisha watoto wote wanapata elimu.

Utekelezaji wa Sheria: Kwa mujibu wa watunga sera, wazazi wanaoshindwa kuwapeleka watoto wao shuleni wanakumbana na adhabu kali ikiwemo kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mpango wa Lishe Shuleni: Serikali imeonesha dhamira yake ya kulinda haki ya elimu kwa watoto wa Tanzania kwa kutekeleza programu za lishe shuleni.

Ufahamu wa Wazazi kuhusu taratibu za Kuripoti Ukiukaji wa Haki ya Elimu

Wazazi walifahamu aina za ukiukaji wa haki ya elimu unaoweza kutokea katika eneo la shule, kama vile ubakaji, adhabu za viboko, na watoto kurudishwa nyumbani kwa kushindwa kulipa karo au michango ya shule. Hata hivyo, matokeo yanatoa picha mchanganyiko kuhusu ufahamu wa taratibu za kuripoti. Kwa ujumla, wazazi walionekana hawafahamu njia na taratibu za kuripoti ukiukwaji wa haki ya elimu.

Ufuatiliaji wa Wazazi wa Maisha ya Kila Siku ya Watoto

Kwa wastani zaidi ya 80% na zaidi ya 78% ya wazazi wenye kipato kikubwa katika makundi tofauti, walijua ni wapi watoto wao wanatumia muda wao mwingi na watoto wanaombatana nao baada ya kutoka shule. Hakukuwa na tofauti katika ufuatiliaji kwa wazazi wote bila kujali hali yao ya kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, wakati wa mahojiano, walimu na viongozi wa jamii walitofautiana na maoni ya wazazi. Walimu walisema kwamba ushiriki wa wazazi kwa shule za sekondari ni mdogo ikilinganishwa na ushiriki kwa shule za awali na msingi.

Wazazi kutoa Mahitaji ya Msingi ili Kuwezesha Elimu ya Watoto wao

Katika muktadha wa Kiafrika, akina baba kwa kawaida ndio wenye wajibu (au wanatarajiwa) kuwasomesha watoto wao. Hata hivyo, ilibainika kuwa baadhi ya akina baba walikuwa hawatekelezi wajibu wao wakiwaachia akina mama mzigo wa majukumu ya kusomesha watoto. Licha ya kipato chao kidogo, akina mama wengi wanahamasa na wamejiandaa kuhakikisha watoto wao wanapata elimu.

Wajibu wa Viongozi wa Jamii na Wanajamii kulinda na kukuza Haki ya Elimu

Jukumu la viongozi wa jamii na wanajamii wenyewe katika kukuza haki ya elimu kwa watoto lilijadiliwa chini ya mada ndogo tatu, uongozi na elimu ya wazazi, wajibu wa jamii kwenye malezi ya watoto, na tabia za watoto na vijana.

Uongozi na kuongeza Uelewa kwa Wazazi: Viongozi wa jamii waliripoti kuwa baadhi ya wanajamii, hasa wazazi, hawajali sana masuala ya elimu.

Wajibu wa Jamii Kulea Watoto: Viongozi walikuwa na wasiwasi kuhusu ongezeko la kutoshirikishwa kwa wanajamii katika kuwalea watoto. Jukumu la kulea watoto linahama taratibu kutoka kuwa la jamii nzima sasa linakuwa la mtu binafsi na familia.

Tabia za watoto: Kuna juhudi zinafanywa kushirikisha zaidi wanajamii ili kuhakikisha watoto wanahudhuria shule na wanajifunza.

Barabara zisizopitika na umbali mrefu iliko shule

Kutopangwa na kutopimwa rasmi kwa mitaa mingi ya watu maskini mjini kumesababisha kuwepo kwa miundombinu duni ya barabara. Hali hii imekuwa kikwazo kwa watoto kwenda shule hasa msimu wa mvua. Pia, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wasichana wako kwenye hatari zaidi ya unyanyasaji wa kijinsia pale wanapolazimika kusafiri umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni, na hii inaweza kusababisha mimba za utotoni na kuacha shule.

Wazazi kuhalalisha unyanyasaji wa kijinsia kwa wasichana

Baadhi ya wazazi waishio makazi yasiyo rasmi ya mijini huwa wanachukulia unyanyasaji wa kijinsia kuwa jambo la kawaida licha ya ukweli kwamba una athari mbaya kwa elimu na afya ya wasichana. Matokeo ya utafiti huu, yameonesha kuwa wazazi hawakuchukua hatua zozote dhidi ya ukatili mbaya wa kingono uliofanywa kwa wanafunzi wa kike kama vile ubakaji. Pia, baadhi ya walimu walibainisha kuwa, wanakosa ushirikiano kutoka kwa wazazi wakati wanafuatilia kesi za ukatili/unyanysaji wa watoto.

Hitimisho

Matokeo yanaonesha kuwa 98.1% ya watoto wanasoma shule, na idadi ya wasichana ni kubwa kidogo kuliko wavulana. Kwa watoto wenye mahitaji maalum ambao ni (2.3% ya jumla), ni 10% tu miongoni mwao ndio wanaosoma shule, jambo linaloonesha bado kuna pengo kubwa la upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum wanaotoka familia zenye kipato duni. Shule sita kati ya kumi (60%) zina huduma kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, na zile ambazo hazina mazingira rafiki kwa watoto wenye ulemavu ziliripoti kuwa ni kutokana na kukosa vifaa. Kwa mwaka wa masomo 2022, wanafunzi wengi katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, na sekondari ya kawaida waliandikishwa kwenye shule za serikali (79.9%, 87.3%, na 90.6%, mtawalia). Miongoni mwa shule zilizofanyiwa utafiti, uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi ulizidi idadi iliyopendekezwa na serikali (watoto 40) katika ngazi zote. Zaidi ya hayo, wastani wa ukubwa wa darasa ulizidi wanafunzi 100 kwa kila darasa kwa shule ya msingi. Hii inaashiria kudhoofisha ubora wa elimu. Mwisho, haki ya elimu imeainishwa katika mada ndogo tatu: sera na mikakati, utekelezaji wa sheria na mpango wa lishe shuleni.

1. Sera na Mikakati: Wadau walipongeza wajibu wa serikali kulinda na kukuza haki ya elimu. Mifano iliyotajwa ni pamoja na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania ya mwaka 2014 (toleo la 2023) ambayo inaeleza mafanikio kwenye utoaji wa elimu ya msingi na sekondari bila ada.

2. Utekelezaji wa Sheria: Mamlaka za serikali za mitaa (Halmashauri) zinahimiza kwa juhudi kubwa wazazi kuwapeleka watoto wao shule.

3. Mpango wa Lishe Shuleni: Dhamira ya serikali kulinda haki ya elimu inajidhihirisha kupitia utekelezaji wa programu zilizopendekezwa za kutoa lishe shuleni.

Mapendekezo Muhimu

i. Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi kwenye makazi yasiyo rasmi nchini Tanzania wanapaswa kuanzisha programu zinazowalenga zaidi watoto kutoka familia maskini kama vile ufadhili wa masomo, mifuko ya kuhimiza usawa kwa kusaidia watoto maskini na vifaa vya kukuza utu na hadhi kwa wasichana.

ii. Kukuza fursa za usawa kwenye shule mchanganyiko na jumuishi, kuna haja ya kuwabaini wanafunzi wenye ulemavu na kuwaandikisha kwenye shule jumuishi na shule mchanganyiko.

iii. Serikali inapaswa kuondoa au kudhibiti malipo ya ziada, michango, na gharama nyingine za elimu zisizo za moja kwa moja ili kuboresha upatikanaji wa elimu na usawa kwa makundi yote ya kijamii na kiuchumi.

iv. Serikali inahitaji kuandaa walimu wengi zaidi wa elimu maalum ili kukidhi mahitaji, pia walimu wa kike waongeze sifa za kitaaluma hadi elimu ya juu kwa ajili ya kufundisha shule ya msingi.

v. Serikali inahitaji kuongeza rasilimali zaidi ili kuziwezesha shule kupata vifaa vya usafi wa mazingira, kulinda afya, maji safi na salama, na vifaa vingine vya kujifunzia.

vi. Kuna haja ya kushughulikia mazingira hatarishi yanayowazunguka watoto: Wanafunzi mara nyingi wanaishi kwenye mazingira yasiyo salama wakiwa wamezungukwa na vilabu vya pombe za kienyeji na takataka zisizoondolewa.

vii. Serikali inapaswa kuajiri walimu wengi zaidi ili kupunguza uwiano mkubwa wa mwalimu kwa wanafunzi, ijenge madarasa kupunguza mlundikano wa watoto darasani na kutoa vitabu vingi vya kiada kwa wanafunzi.

viii. Shule ziandae vikao vya kielimu kwa wazazi ili kujenga uelewa kwa wazazi kuhusu wajibu wao kushiriki kikamilifu kwenye masuala ya ujifunzaji wa watoto wao, hasa wazazi/walezi wa kiume.

ix. Wathibiti ubora wa shule na Maafisa Afya wanapaswa kutembelea shule mara kwa mara bila kutoa taarifa ili kukagua na kuhakikisha viwango vya kitaaluma na afya vinadumishwa siku zote.

x. Kuna haja ya kutoa elimu ya uraia kwa viongozi wa mitaa, na wanajamii ili kwa pamoja waweze kushughulikia baadhi ya matatizo au vikwazo kwa watoto kujifunza kwa ufanisi.

xi. Serikali na wadau wa elimu wajikite kutoa fursa za elimu endelevu ndani ya mfumo wa elimu.

Rejea

Adams, J., Bartram, J., Chartier, Y., & Sims, J. (2009). Water, sanitation and hygiene standards for schools in low-cost settings: World Health Organization.

Alfonso Echazarra & Thomas Radinger, (2019). "Does attending a rural school make a difference in how and what you learn?," PISA in Focus 94, OECD Publishing

Alisha M. B. Braun (2022) Barriers to inclusive education in Tanzania's policy environment: national policy actors' perspectives, Compare: A Journal of Comparative and International Education, 52:1, 110-128, DOI: 10.1080/03057925.2020.1745057

Bashman, L. E. (2008). Perspectives of Teachers on the problem of child sexual abuse in squatter camp. Nelson Mandela University. Retrieved from: http://hdl.handle.net/10948/684

Crawfurd, L., Hares, S., & Todd, R. (2023). The Impact of Private Schools, School Chains and PPPs in Developing Countries. The World Bank Research Observer, Ikad005.

Deogratias, E. (2024). Forecasting Students' Enrolment in Tanzania Government Primary Schools from 2021 to 2035 Using ARIMA Model: Forecasting Students' Enrolment in Tanzania. International Journal of Curriculum and Instruction, 16(1), 162-174

Desai, S. (2018). World Development Report 2018: Learning to Realize Education's Promise.

Ginsburg, M., Haugen, V., Lokong, F., & Ong'uti, S. (2017). Promoting community participation in improving education in South Sudan. African Educational Research Journal, 5(4): 221-239.

Hife, L., & Pañares, N. (2023). Parental Involvement and Mathematics

Academic Performance of Grade 2 Learners. International Journal of Research Publications, 129(1).

Khusheim, S. M. (2022). Students with Special Educational Needs: Explaining Their Social Integration and Self-Concept. Journal of Education and Learning, 11(1), 54-64.

Khusheim S.M. (2021). Students with Special Educational Needs: Explaining Their Social Integration and Self-Concept. Journal of Education and Learning; Vol. 11, No. 1; 2022

Lindsjö, K. (2018). Contextualizing the quality of primary education in urban and rural settings: The case of Iringa Region, Tanzania. Norsk Geografisk Tidsskrift-Norwegian Journal of Geography, 72(4), 234-247.

Lukindo, J. J. (2018). Contribution of school feeding programmes (sfps) in enhancing pupils'schooling in primary schools in monduli district, tanzania. European Journal of Education Studies.

Lupala, J. M. (2014). The social dimension of sustainable development: Social inclusion in Tanzania's Urban centres. Current Urban Studies, 2(04), 350.

Maemeko ,E & Mukwambo, M & Nkengbeza, D (2021). Social Challenges Learners Residing in Informal Settlements in Katima Mulilo Town Face in Learning. Journal of Curriculum and Teaching, 10 (3) pp36-46

Magina, F. B., Kyessi, A., & Kombe, W. (2020). The urban land nexus–challenges and opportunities of regularising informal settlements: The case studies of Dar es Salaam and Mwanza in Tanzania. Journal of African Real Estate Research, 5(1), 32-54.

Maliti, E. (2019). Inequality in education and wealth in Tanzania: A 25-year perspective. Social Indicators Research, 145(3), 901-921 Mlawa, K. P. and Mtitu, E. A.. (2022). Perception of School

Stakeholders on Shadow Education in Iringa Municipality, Tanzania. East African Journal of Education and Social Sciences 3(1), 89-93. Doi: https://doi.org/10.46606/eajess2022v03i01.0150

Mannion, G., & Sowerby, M. (2018). Learner Participation in Educational Settings (3-18).

Msafiri, D. (2023a). Gender balance in Tanzania: Success and challenges. REPOA Brief.

Mligo, I. (2018). Enhancing Young Children's Access to Early Childhood Education and Care in Tanzania. InTech. doi: 10.5772/intechopen.71265

National Buerau of Statistics. (2019). Household Budget Survey 2017-18: Key Indicators Report.

Oketch,M. & Ngware ,M.W (eds.) (2012).urbanization and Education in East n Africa: African Population and Health Research Center. ISBN 978-9966-21-175-0.

Right to Education Initiative (RTE)2023, Right to Education n Initiative's contribution to the UN Special Rapporteur on the right to education's report on the right to education, advances and challenges

Roy, M., Shemdoe, R., Hulme, D., Mwageni, N., & Gough, A. (2018). Climate change and declining levels of green structures: Life in informal settlements of Dar es Salaam, Tanzania. Landscape and Urban Planning.https://doi.org/10.1016/j.landurbplan.2017.11.011

Roy, M., Shemdoe, R., Hulme, D., Mwageni, N., & Gough, A. (2018). Climate change and declining levels of green structures: Life in informal settlements of Dar es Salaam, Tanzania. Landscape and Urban Planning, 180, 282-293. Shao, T., Zhao, J., Hu, H., & Zhang, Q. (2021). Analysis of factors affecting students going to school toilets in a rural primary school in China. BMC Public Health, 21, 1-11.

StudyCorgi (2023). 21st Century Skills that every Learner Needs. Retrieved on September 7, 2023 from: https://studycorgi.com/blog/21st-century-skills-that-every-learner-needs/

Sumida, S., & Kawata, K. (2021). An analysis of the learning performance gap between urban and rural areas in sub-Saharan Africa. South African journal of education, 41(2), 1-17.

Tieng'o E.W (2020). Perception of School Management Committees on Community Participation in Education among Primary Schools in Tanzania. East African Journal of Education and Social Sciences EAJESS July-September 2020, Vol. 1, No. 2, pp. 128-140

The Citizen (April 12, 2021). Teacher-student ratio still a concern. Retrieved on September 5, 2023 from: https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/national/teacher-student-ratio-still-a-concern-2636160

UNESCO Institute for Statistics. (2015). A growing number of children and adolescents are out of school as aid fails to meet the mark. Available at: https://en.unesco.org/gem-report/growingnumber-children-and-adolescents-are-out-school-aid-fails-meet-mark

UNESCO (2021).Global Education Monitoring Report 2021/2: Non-state actors in education: Who chooses? Who loses? Paris, UNESCO.

UNESCO Institute for Statistics (2016). The World needs almost 69 million new teachers to reach the 2030 education goals

UNESCO 2019, the right to education handbook, UNESCO, https

UNICEF (2021). A situation analysis of Children and Young People with Disabilities in Mainland Tanzania and Zanzibar. UNICEF. Available at https://www.unicef.org/tanzania/reports/children-and-young-people-disabilities-tanzania

Wang, H., & Chow, S. C. (2007). Sample size calculation for comparing proportions. Wiley Encyclopedia of clinical trials, 10,

9781118445112.

Williams (2019). High-achieving, low-income students' perspectives of how schools can promote the academic achievement of students living in poverty. SAGE

Worrall, L., Colenbrander, S., Palmer, I., Makene, F., Mushi, D., Mwijage, J., Martine, M., and Godfrey, N., 2017. Better Urban Growth inTanzania: Preliminary Exploration of the Opportunities and Challenges. Coalition for Urban Transitions, London and Washington, DC.

Woodcraft, S., Osuteye, E., Ndezi, T., & Makoba, F. D. (2020). Pathways to the 'good life': Co-producing prosperity research in informal settlements in Tanzania. Urban Planning, 5(3), 288-302.

Zhang, B., Zhou, Y., Jiang, Y., Zheng, C., Li, H., & Lan, S. (2023). Determinants of Preschool Choice: Understanding How Middle-income Parents Choose Kindergartens in Shanghai. Journal of Child and Family Studies, 32(4), 989-1001

HakiElimu

Mathuradas Road off UN Road.
Plot Number 739
S.L.P 79401, Upanga, Ilala
Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 (0)22 2151852/3
Fax:+255 (0)22 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.or.tz
Tovuti: www.hakielimu.or.tz

African Population Health Research Center

S.L.P 10787- 00100
APHRC Headquarters, Kitisuru,
Nairobi, Kenya
Baruapepe: info@aphrc.org

Simu: +254 (20) 400 1000, 266 244 or 266 2255
Simu: +254 722 205 933, 733 410 102
Fax:+254 (20) 400 1101